# Taarifa ya Uhamiaji & *Visa* kwa Waathiriwa wa Dhuluma za Kimapenzi & Baina ya Watu

Wanafunzi na wasomi kutoka mataifa mengine walio na maswali kuhusu hadhi yao ya uhamiaji na *visa* wanashauriwa kutafuta usaidizi wa mwanasheria wa uhamiaji. Waraka huu ni rasilimali ya kuelezea vipengele fulani vya sheria, lakini hauchukui nafasi ya ushauri wa kisheria.

**Nimekuwa mwathiriwa wa shambulizi, je, hadhi yangu ya uhamiaji inaathiri uwezo wangu wa kufikia rasilimali zilizo ndani ya bewa?**

La. Chini ya sheria, wanafunzi na wafanyikazi ambao ni waathiriwa au manusura wa dhuluma za kimapenzi na za baina ya watu wana haki sawia chini ya Kifungu cha IX cha Marekebisho ya 1972 ya Sheria ya Elimu (Kifungu cha IX) na Sheria ya Dhuluma dhidi ya Wanawake (VAWA), bila kujali hadhi ya uhamiaji au *visa* .

Taarifa kuhusu rasilimali za kimatibabu na ushauri ndani ya bewa, na vile vile malazi yanayopatikana, zinaweza kupatikana kwenye: https://1is2many.okstate.edu/

Taarifa kuhusu mchakato wa kinidhamu wa wanafunzi zinaweza kupatikana kwenye: https://studentconduct.okstate.edu/code

Chuo hakitalipiza kisasi dhidi yako au kukuchukulia tofauti kwa msingi wa kuripoti tendo la jinai.

**Je, ninaweza kuandikisha mashtaka kama mhamiaji aliyesajiliwa au ambaye hajasajiliwa?**

Ndiyo. Taarifa kuhusu fafanuzi za jinai za jimbo lako za shamulizi la kimapenzi, dhuluma za kinyumbani, dhuluma za uchumba na ufuatiliaji mtu kwa njia isiyo ya kawaida zinaweza kupatikana katika Ripoti ya kimwaka ya Usalama: https://police.okstate.edu/annual-security-reports

Maswali mahsusi kuhusu kuandikisha mashtakayanaweza kutumwa kwa :

Oklahoma State University Police Department, OSUPD
104 USDA Building, Stillwater, Oklahoma 74078
405-564-6523
https://police.okstate.edu/
1is2many@okstate.edu

**Je, kuna hadji mahsusi za *visa* na uhamiaji kwa waathiriwa wa matendo ya jinai?**

Ndiyo. Kwa waathiriwa wa shambulizi la kimapenzi, dhuluma za kinyumbani, dhuluma za uchumba na ufuatiliaji mtu kwa njia isiyo ya kawaida, huenda kukawa na chagiuo zingine za *visa* , ikiwa ni pamoja na *Visa* za U na T. Kwa maelezo, zungumza na mwanasheria wa uhamiaji.

| ***Visa* ya U** | ***Visa* ya T** |
|---|---|
| Kwa waathiriwa wa mashambulizi mabaya ya kimwili au kiakili kutokana na shughuli fulani ya kijinai, ikijumuisha shambulizi la kimapenzi, dhuluma za kinyumbani, kunajisiwa, mashambulizi, au matendo mengine husika ya jinai<br>-Mwathiriwa/mtuma ombi ni lazima awe mwathiriwa wa shughuli ya kijinai inayohitimu na ana uwezekano wa kusaidia katika uchunguzi na/au kufungulia shughuli hiyo ya kijinai mashtaka<br>-Kwa ujumla ni halali kwa miaka minne<br>-Kwa taarifa zaidi, shauriana na mwanasheria wa uhamiaji, na utazame:<br><br>http://www.uscis.gov/humanitarian/victims-human-trafficking-other-crimes/victims-criminal-activity-u-nonimmigrant-status/victims-criminal-activity-u-nonimmigrant-status | Kwa waathiriwa wa ulanguzi wa binadamu<br>-Ni lazima ukubali maombi kutoka kwa mamlaka za utekelezaji sheria ya ushirikiano katika uchunguzi au kufungulia mashtaka tendo/matendo ya ulanguzi (isipokuwa uwe hauwezi kushirikiana kwa sababu ya kudhoofika kimwili au kiakili), na ni lazima uweze kuonesha kwamba mwathiriwa/mtuma ombi anaweza kupitia hali ngumu sana akiondolewa Marekani<br>-Kwa ujumla ni halali kwa miaka minne<br>-Kwa taarifa zaidi, shauriana na mwanasheria wa uhamiaji, na utazame:<br><br>http://www.uscis.gov/humanitarian/victims-human-trafficking-other-crimes/victims-human-trafficking-t-nonimmigrant-status |

**Je, kuna ofisi ndani ya bewa inayoweza kunipa taarifa za ziada?**

, International Students & Scholars
250 Student Union, Stillwater, OK 74078
405-744-5459
https://lcl.okstate.edu/iss/
su-iss@okstate.edu

Ofisi ya Wanafunzi na Wasomi kutoka Mataifa Mengine inaweza kutoa taarifa muhimu kuhusiana na hadhi ya uhamiaji. Kumbuka kwamba kwa maswali yanayohusiana na mabadiliko kwa hadhi nyingine za uhamiaji, au chaguo za kisheria zilizo nje ya visa wastani za wanafunzi za F-1 na J-1, au visa za kazi zinazosimamiwa na mwajiri, shauriana na mwanasheria wa uhamiaji aliyehitimu..

| **Chaguo za *Visa*** |
|---|

SUNY The State University of New York

| Wanafunzi wenye hadhi za F-1 na J-1 | Waajirwa wa H-1B, O-1, E-3, au TN |
|---|---|
| • Chaguo za idhini iliyopunguzwa ya masomo kwa ajili ya hali za kimatibabu zilizothibitishwa na daktari wa kimatibabu mwenye leseni, daktari wa osteopathia, au mwanasaikolojia kwa kimatibabu mwenye leseni<br>• Chaguo za, na madhara ya, kujiondoa kwenye masomo yako<br>• Taarifa kuhusu kurejea kwenye masomo siku za baadaye, mwanafunzi akiamua kujiondoa<br>• Chaguo na madhara ya wanandoa wanaoandamana<br>• Taarifa jumla kuhusu chaguo za kubadilisha hadhi ya visa.<br>• Taarifa jumla kuhusu *visa* za U na T. (Kutumwa kwa mwanasheria wa uhamiaji aliyehitimu)<br>• Kutumwa kwa mwanasheria aliyehitimu | • Chagu za ruhusa ya kutokuwa kazini, na madhara kwa hadhi yako ya uhamiaji<br>• Chaguo na madhara ya wanandoa wanaoandamana<br>• Taarifa jumla kuhusu chaguo za kubadilisha hadhi ya visa. Kutumwa kwa mwanasheria wa uhamiaji aliyehitimu<br>• Taarifa jumla kuhusu *visa* za U na T. (Kutumwa kwa mwanasheria wa uhamiaji aliyehitimu)<br>• Kutumwa kwa mwanasheria wa uhamiaji aliyehitimu<br>• Waakazi wa kudumu wa Marekani waliosubirishwa (green card bado haijaidhinishwa)<br>• Athari ya kuondoka kwenye ajira yako ukiwa kwenye ombi la mkaazi wa kudumu linalosimamiwa na mwajiri wako;<br>• Kutumwa kwa mwanasheria aliyehitimu |

**Je, mwanasheria wa uhamiaji ni nani na kazi yake ni gani?**

Mawakili wa uhamiaji ni wanasheria wenye leseni wenye utaalamu katika nyanja ya sheria ya uhamiaji. Wanatenda kama watetezi wa mteja, na wanaweza kuwawakilisha mbele ya mashirika ya uhamiaji, katika mahakama za uhamiaji na vile vile katika kutuma maombi ya manugaa ya uhamiaji, Wakili huyu anaweza kutoa ushauri jumla na anaweza kujadili chaguo za uhamiaji, Kama tu mawakili wote, mawakili wa uhamiaji wako chini ya mahitaji ya maadili ya kitaalamu na kisheria, na wanaweza majadiliano ya wateja kwa usiri.

**Je, ninaweza kumpata wapi mwanasheria wa uhamiaji wa ndani?**

| | |
|---|---|
| Huduma za Uraia na Uhamiaji za Marekani (USCIS), ofisi ya Idara ya Usalama wa Ndani (DHS), inatoa tovuti mbili za kuwasaidia watu kupata uwakiliho wa kisheria wa bila malipo au gharama ya chini:<br>USCIS: Pata Usaidizi katika Ukurasa wa Tovuti wa Jamii yako | <br>USCIS: Pata Ukurasa wa Tovuti wa Huduma za Kisheria |
| Bodi ya Rufaa za Uhamiaji (BIA) inatoa orodha ya wanasheria katika kila jimbo wanaotoa huduma za uhamiaji bila malipo au kwa gharama ya chini | |
| Chama cha Mawakili wa Uhamiaji cha Marekani (AILA) kinatoa Huduma ya Kuwapendekeza Mawakili ya mtandaoni inayoweza kumsaidia mwanafunzi au msomi kupata wakili wa uhamiaji. | |
| Chama cha Mawakili cha Marekani pia kinatoa taarifa kuhusu kupata huduma za kisheria katika kila jimbo. | |